



Mizizi na mbevu za pungapunga (sapi) Punga zeze



Ndago (*Cyperus spp*)



Morning glory (*Ipomoea aquatica*)



Shamba la mpunga lenye magugu



Shamba la mpunga lisilo na magugu

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Meneja wa Kituo
TARI Dakawa
S.L.P 1892, Morogoro, Tanzania
Simu: (+255) 23 2934300,
Baruapepe: cmdakawa@tari.go.tz

Kimetayarishwa na:
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
KITUO CHA DAKAWA



TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
(TARI)

MAGUGU SUMBUFU
KATIKA ZAO LA MPUNGA



 @Tari tv
 @Tari Tanzania
 @tari

UTANGULIZI.

Magugu ni mimea isiyofaa, inaharibu na inaingilia ukuaji wa mimea mingine ya mazao. Athari za magugu kwa zao la mpunga ni pamoja na kushindana na mpunga kwa mwanga, maji na lishe, kupunguza ubora na wingi wa mazao, ufanisi wa mbolea na kuongeza gharama kwenye uzalishaji. Pia magugu huwa ni maficho ya wadudu na vimelea vya magonjwa.

AINA ZA MAGUGU YANAYOPATIKANA KWA WINGI KATIKA MASHAMBA YA MPUNGA

- i. Limbwaga. Water grass (*Echinochloa spp*)
- ii. Punga pori
 - a. Punga punga/sapi (*Oryza longistaminata*)
 - b. Punga zeze (*Oryza punctata*)
- iv. Ukoka/mbudu (*Cynodon dactylon*)
- v. Ndago (*Cyperus Spp*)
- vi. Gugu karanga (*Marsilea minuta*)
- vii. Morning glory (*Ipomoea aquatic*)
- viii. Gugu kuwasha/gugu kata (*Rottboellia cochinchinensis*)



Gugu Limbwaga Water grass (*Echinochloa spp*)



Gugu kuwasha/gugu kata (*Rottboellia cochinchinensis*)

UDHIBITI WA MAGUGU

Njia za kudhibiti magugu

Kuna njia kuu tatu za kudhibiti magugu shambani:

- Kutumia mikono/jembe la mkono
- Kutumia zana za kupalilia
- Kupalilia kwa kutumia kemikali (viua gugu)

Mbinu za Kuzuia na Kudhibiti magugu shambani

a. Udhhibiti wa moja kwa moja

- Kulima kilimo cha mzunguko hasa kuhusisha mazao yasiyotegemea maji mengi ili kupunguza benki ya mbegu za magugu kwenye ardhi
- Kupalia kwa mikono au jembe la mikono katika hatua za awali za uotaji
- Kufurisha maji
- Kutumia viua-gugu
 - o Kabla ya kupanda
 - o Baada ya kupanda



Gugu karanga (*Marsilea minuta*)



Ukoka (mbudu) (*Cynodon dactylon*) na couch grass

b.Udhibiti wa magugu kwa njia ya kuzuia

- Tumia mbegu safi toka chanzo kinachoaminika na zilizothibitishwa
- Kusafisha mara kwa mara zana na mashine za shambani kuzuia kuendelea kusambaza mbegu toka mashamba mengine
- Usimamizi mzuri wa kulima, tarehe za kupanda, namna ya kupanda, aina ya mbegu itakayopandwa, nafasi ya kupanda na matumizi ya mbolea unasaidia mimea kuota na kustawi vizuri na kuyazuia magugu mengi na hivyo kupunguza mahitaji ya baadhi ya mbinu za kupambana na magugu
- Panda kwa kutumia mistari ili kuweza kutambua na kuyaondoa magugu kirahisi
- Andaa shamba vizuri kupunguza wingi wamagugu
- Safisha mifereji ya maji ya kumwagilia namajaruba
- Zuia vipande vya mimea ambayo ni magugu kuingia shambani kwa njia ya maji
- Tumia njia za kiasili kama vile mzunguko wa mazao, panda mazoa funika, kuwa na idadi sahihi ya mimea shambani na kupanda kwa mistari
- Ingiza maji shambani kabla ya msimu ili magugu yaote kisha kuyaangamiza wakati wakulima
- Chagua na lima aina ya mpunga wenye uwezo mkubwa wa kuota na kupacha haraka ili kushindana na magugu 30
- Kupalilia kwa mashine na vifaa rahisi mfano, kutumia vipalizi (weeders; rotary na cono weeder), kung'olea kwa mikono
- Udhhibiti magugu kibailojia: Hii inahusisha kutumia viumbe hai kama vile wadudu, vimelea vinavyosababisha magonjwa, viumbe walao majani ya magugu mfano, Samaki
- Mbinu shirikishi (Integrated weed management (IWM): Inahusisha dhana ya kutumia mbinu nyingi za kudhibiti magugu kwa kufanya idadi ya magugu isiwe na madhara kiuchumi na wakati huo huo kulinda ubora wa mazingira.